



## KONGAMANO LA ISHIRINI NA NNe LA KISWAHILI

### Bayreuth, tarehe 3 hadi tarehe 5 mwezi wa sita 2011

Tarehe 4, mwezi wa tano,  
mwaka wa 2011

Wapendwa Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Leo tunawaletea barua ya pili ya mwaliko ikiambatanishwa na ratiba yetu ya Kongamano. Mwaka huu tena, kongamano litafanyika siku tatu katika jengo la 'Iwalewa-House' (Münzgasse 9, tazama ramani kwenye ukurasa wa pili). Kongamano litaanza **Ijumaa taraha 3 mwezi wa sita** kuanzia **saa mbili na nusu asubuhi**. Kutakuwa na malipo ya usajili ya €6 kwa wasio wanafunzi na €3 kwa wanafunzi.

Tunawaomba wale ambao wajatupatia mada yao, watuandikie. Tena tunawaomba wote watakaoandika makala zao kwa Kiswahili waandike kifupisho cha makala kwa Kiingereza, watupatie kwa [swahili@uni-bayreuth.de](mailto:swahili@uni-bayreuth.de) (siku ya mwisho iwe **tarehe 25**, mwezi wa tano).

Kwa sababu mara hii makala tulizozipokea ni nyingi mno muda wa kutoa makala utakuwa **dakika 20** na **dakika 5** za kujadili kila wasilisho la makala.

Ziada ya kuwa na filamu tatu, tutakuwa na hafla mbili nyingine maalum: siku ya Ijumaa, tutafungua maonyesho "Von einem Ufer zum anderen – die Karawanenroute Sansibar-Tanganyikasee" ("From one shore to the other – the caravan route Zanzibar –Lake Tanganyika") yatakayoletwa na Thomas Dorn na Nathalie Carré waliofuata nyayo za akina Tippu Tip kutoka Unguja mpaka Kigoma. Siku ya Jumamosi, wanamuziki watatu kutoka Cologne (M.U.T.) watapiga muziki, mchanganyiko wa jazz na muziki kutoka Argentina na Turkiya.

Kabla Kongamano la Kiswahili halijaanza, wageni na wenyeji wote wanaombwa wakutane pamoja tarehe **2 mwezi wa sita, saa moja jioni** katika mkahawa unaoitwa '**Delphi**' uliopo katika Badstr. 14 (tazama ramani). Huko kutakuwa na chakula na vinywaji ambavyo watakaohudhuria watajinunulia wao wenyewe.

Muda si mrefu tutawaandikia wale wanafunzi ambao wanataka kupata malazi kwa wanafunzi wengine wa Bayreuth.

Karibuni sana Bayreuth. Wenu wakweli,

Prof. Gabriele Sommer, Dr. des. Clarissa Vierke,  
Afrikanistik I  
Universität Bayreuth,  
95440 Bayreuth  
Tel.: +49-921-553556  
Fax.: +49-921-553627

Prof. Said A. M. Khamis  
Literaturen in afrikanischen Sprachen  
Universität Bayreuth,  
95440 Bayreuth  
Tel.: +49-921-553598  
Fax.: +49-921-553641

